**SHAREHOLDERS FREQUENTLY ASKED QUESTIONS (FAQs).**

1. **Mwanahisa: Kwanini tangu ninunue hisa mwaka 2011, sijawahi kusikia chochote kuhusu maendeleo ya kampuni?**

   **Kampuni**: Kampuni huwasiliana na wanahisa wake kwa njia moja kuu ambayo ni kupitia Mkutano wa Wanahisa. Mkutano huu hufanyika kila mwaka. Baada ya Kampuni kufunga mwaka wake wa fedha (Tarehe 31, Machi) na hesabu zake kukaguliwa na Mkaguzi wa nje na kuthibitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni, Kampuni hutoa notisi ya Mkutano Mkuu kwa Wanahisa wake.

   Kampuni yetu imekuwa ikitoa notisi hizi kupitia magazeti ya Kiswahili na kiingereza, walau mara mbili kwa kila gazeti, siku zisizopungua ishirini na moja kabla ya tarehe ya Mkutano.

   Kupitia Mkutano Mkuu wa Wanahisa, Wanahisa wa Kampuni yetu;

   (a) hupokea taarifa ya Kampuni kutoka kwa Bodi ya Wakurugenzi,

   (b) hujadili na kupitisha mipango mbalimbali ya Kampuni,

   (c) hupokea, kujadili na kuthibitisha taarifa ya ukaguzi wa fedha wa mwaka,

   (d) huchagua na kuthibitisha wakurugenzi wa Kampuni na kupitisha malipo yao, na

   (e) huteua na kuthibitisha wakaguzi wa nje wa Kampuni na kupanga malipo yao.

   Katika Mkutano Mkuu wa Wanahisa, Wanahisa wa Kampuni yetu pia hupata nafasi ya kujadili taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi kuhusu maendeleo ya Kampuni na kuhoji mada yoyote ikiwemo kutoa ushauri kwa kampuni kuhusu utekelezaji wa mipango yake.

   Mwanahisa aweza kumchagua mtu yeyote (Mwenye umri wa miaka 18 na zaidi) kumuwakilisha katika Mkutano Mkuu wa Wanahisa kwa kujaza fomu ya uwakilishi

(inayopatika katika tovuti ya Kampuni) na kuiwasilisha fomu hiyo katika ofisi ya Kampuni, ikiwemo ofisi zake za mauzo, siku saba kabla ya Mkutano.

Pia, kwa Mwanahisa ambaye hawezi kwa sababu zozote kuhudhuria Mkutano wala kumtuma muwakilishi, aweza kupata taarifa za Mkutano katika tovuti ya Kampuni au katika ofisi zetu.

Kampuni yetu imekuwa ikiendesha Mkutano Mkuu wa Wanahisa kwa utaratibu ulioelezwa hapo juu na Mkutano wake wa Mwisho ulifanyika tarehe 29, Agosti, 2016 ikiwa ni Mkutano wake wa Nne (4) wa Mwaka. Pia kupitia Mkutano huu, Mkutano uliridhia Wanahisa kutumiwa taarifa ya Mkutano kupitia namba zao za simu na pia katika tovuti ya Kampuni.

2. **Mwanahisa: Kwa nini kampuni haijawahi kutoa gawio?**

   **Kampuni:** Kampuni kupitia Mkutano Mkuu wa Wanahisa, hutangaza gawio baada ya kuzingatia maoni ya Bodi ya Wakurugenzi. Kwa kawaida, kampuni hutoa gawio kwa Wanahisa baada ya kutangaza faida katika kufunga mwaka wake wa fedha. Kwa mfano: iwapo maendeleo ya Kampuni sio mazuri kifedha au iwapo kampuni imepata hasara, Bodi ya Wakurugenzi inaweza kushauri Mkutano kutotangaza gawio kwa Wanahisa. Pia hata kama faida imepatikana, Bodi inao uwezo wa kushauri Mkutano Mkuu wa Wanahisa kutotangazwa au kutolewa kwa gawio na kushauri faida iliyopatikana kuingizwa tena katika mtaji wa kampuni kuendeleza kampuni zaidi.

   Kutokana na Kampuni yetu kutofanya vizuri na pia kutokana na kampuni kulimbikiza madeni mengi, Kampuni haijawahi kutoa gawio kwa Wanahisa wake toka mwaka 2011. Kampuni imeendelea na inaendelea kutekeleza mpango wake mkuu wa kubana matumizi yake na kupanua wigo wa biashara ili kupata faida na hivyo Wanahisa kuweza kufaidika na uwekezaji wao.

3. **Mwanahisa: Mkutano Mkuu wa Mwanahisa hufanyika mara ngapi kwa mwaka na lini (kipindi gani cha mwaka)?**

   **Kampuni:** Mkutano Mkuu wa Wanahisa hufanyika mara moja tu kwa Mwaka, ndio maana Mkutano huu huitwa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa. Mkutano huu hauna kipindi maalum kwa sababu hutegemea taarifa ya Wakaguzi wa nje wa hesabu za Kampuni. Baada ya Wakaguzi wa nje wa hesabu za kampuni kukagua na kupitisha mahesabu hayo, Mahesabu hayo hupelekwa katika Mkutano wa Bodi kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa. Baada ya Bodi kupitisha mahesabu ya kampuni, Bodi hupanga

tarehe ya Mkutano na humuagiza Katibu wa Kampuni kutoa notisi ya Mkutano kwa Wanahisa.

4. **Mwanahisa: Je, utaratibu wa kuhudhuria Mkutano ukoje kwa Kampuni au Taasisi ambayo ni Mwanahisa katika Kampuni ya Precision Air?**

   **Kampuni:** Kutokana na Waraka wa Kampuni yetu (*Memorandum and Articles of Association*) ya Mwaka 1991, (kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2011), Taasisi yoyote ambayo ni Mwanahisa katika kampuni yetu hutakiwa kupitisha azimio kwa maandishi katika Mkutano wa Wanahisa/ Wakurugenzi wake na kumchagua muwakilishi atakayeiwakilisha taasisi hiyo katika Mkutano wa Wanahisa wa Precision Air.

   Azimio hilo yatakiwa kuwa na muhuri wa taasisi hiyo na kuwasilishwa kwa Katibu wa Kampuni siku saba kabla ya Mkutano Mkuu wa Wanahisa. Pia azimio hilo yatakiwa kuelezea kwa uwazi kuhusu msimamo wa taasisi hiyo katika agenda mbalimbali za Mkutano Mkuu wa Wanahisa. Mfano wa azimio hupatikana katika tovuti ya kampuni.

5. **Mwanahisa: Utaratibu ukoje nikitaka kuacha kuwa Mwanahisa?**

   **Kampuni:** Kwa jinsi mwanahisa alivyojiunga na Kampuni kwa kununua hisa kwa mapenzi yake mwenyewe bila kushurutishwa, Mwanahisa pia anayo haki ya kuacha kuwa Mwanahisa. Kutokana na waraka wa Kampuni, mtu yeyote anaweza kukoma kuwa Mwanahisa kutokana na kifo au kwa kuuza/ kuhamisha hisa zake kwa mtu mwingine.

   **Utaratibu wa kuhamisha/ kuuza (*transfer*) hisa ni wa mtu binafsi kupitia mawakala wa soka la hisa (wala sio kampuni ya Precision Air)**. Baada ya kuhamisha huko, rekodi hizo hutumwa katika soko la hisa kwa ajili ya Kumbukumbu. Kampuni yetu haihusiki katika zoezi hili.

   Baada ya zoezi kukamilika na kupitishwa na soko la hisa, Kampuni yetu hujulishwa na soko la hisa kuhusu mauziano hayo na kutumiwa taarifa za Mwanahisa mpya.

6. **Mwanahisa: Je Kampuni bado inaendelea kuuza hisa zake?**

   **Kampuni**: Hapana, Kampuni iliuza hisa zake mara moja tu katika soko la awali (*Initial Public Offering/ primary market*). Kwa sasa kinachoendela katika soko la hisa ni mauziano baina ya Wanahisa na wanunuaji wengine wa hisa kupitia Mawakala wa soko la hisa la Dar es Salaam ( *yaani Secondary Market*).

7. **Mwanahisa: Je naweza kurudishiwa fedha zangu nikiamua kuacha kuwa Mwanahisa?**

   **Kampuni**: Hapana, Kampuni yetu haina utaratibu na haiwezi kurudisha fedha kwa Mwanahisa endapo anaamua kuacha kuwa Mwanahisa. Utaratibu huu pia hautambuliki kisheria. Mwanahisa anayo haki ya kuuza hisa zake kupitia utaratibu unaotambulika kisheria ambao ni uuzaji kupitia Mawakala wa soko la hisa.

   Wanahisa wetu wote humiliki hisa za kawaida (*Ordinary shares*) na sio hisa zinazoweza kukombolewa kwa Mwanahisa kurejeshewa fedha zake baada ya muda flani (*redeemable shares*).

8. **Mzazi wangu/ Ndugu yangu alikuwa Mwanahisa wa kampuni ila kwa sasa amefariki, utaratibu ukoje kwa hisa zake?**

   **Kampuni**: Iwapo Mwanahisa atafariki, hisa zake zitarithishwa kisheria (*Transmission of shares*) kwa kufuata sheria na taratibu za mirathi za Nchi kama inavyofanyika kwa mali zake zingine kama kiwanja, shamba, mafao, gari n.k.

   Baada ya Msimamizi wa Mirathi kuchaguliwa katika kikao cha ukoo au kupitia wosia wa Marehemu na Msimamizi huyo kupitishwa na Mahakama kwa maandishi, Msimamizi huyo atatakiwa kuwasilisha barua yake ya usimamizi uliotolewa na Mahakama katika Soko la Hisa la Dar es Salaam kwa utaratibu wa kuhamisha hisa hizo.

9. **Mwanahisa: Je hisa zinahamishika/ Utaratibu ukoje nikitaka kuuza au kuhamisha hisa zangu?**

   **Kampuni**: Ndio, hisa zinahamishika, Mwanahisa aweza kuhamisha hisa zake kisheria kwa mtu mwingine. **Utaratibu wa kuhamisha/ kuuza (*transfer*) hisa ni wa mtu binafsi kupitia mawakala wa soka la hisa (wala sio kampuni ya Precision Air)**. Baada ya kuhamisha huko, rekodi hizo hutumwa katika soko la hisa kwa ajili ya Kumbukumbu. Kampuni yetu haihusiki katika zoezi hili.

   Baada ya zoezi kukamilika na kupitishwa na soko la hisa, Kampuni yetu hujulishwa na soko la hisa kuhusu mauziano hayo na kutumiwa taarifa za Mwanahisa mpya.

10. **Mwanahisa: Iwapo kampuni haipati faida, mustakabali wangu kama Mwanahisa unakuwaje?**

    **Kampuni**: Biashara ya uwekezaji kupitia hisa una faida na changamoto/ hasara zake. Bei za hisa zinapopanda ni faida kwa Mwanahisa kwa sababu huweza kuuza hisa zake kwa faida na vivyo hivyo, bei zikishuka ni hasara kwa Mwanahisa kwa sababu hupata

changamoto katika kuuza hisa zake. Kupanda na kushuka kwa bei za hisa sokoni hutegemea mambo mengi ikiwa ni pamoja na utendaji wa kampuni.

Kampuni ikipata faida, Mwanahisa hufaidika pia kwa kupata gawio, ila Kampuni ikipata hasara, Mwanahisa pia huguswa na hasara hii kwa sababu hapati gawio lolote. Hii ni changamoto ambayo mara Mwahisa anapoamua kununua hisa anapaswa kuelewa.

**11. Mwanahisa: Je ni kwa vipi naweza kupata taarifa za maendeleo ya kampuni?**

**Kampuni**:Taarifa za maendeleo ya Kampuni hupatikana katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa. Pia taarifa hizi hupatika ofisi mbalimbali za Kampuni na katika tovuti ya kampuni: www.precisionairtz.com, (Baada ya kufungua tovuti hii nenda katika sehemu ya "*About us*" katika Menu, bonyeza "*investor Relations*" na uchague taarifa unayoitaji).

**12. Mwanahisa: Mikutano ya Kila mwaka ya Wanahisa hufanyika wapi?**

**Kampuni**: Sehemu/ Eneo la Mkutano Mkuu wa Wanahisa huchaguliwa na Bodi ya Wanahisa kwa kuzingatia mambo mbalimbali ikiwemo uwingi wa wanahisa, uwepo wa miundombinu ya kukidhi mahitaji ya Mkutano n.k.

Kuanzia mwaka 2012, Kampuni yetu imekuwa ikifanya Mikutano yake katika jiji la Da es Salaam. Katika Mikutano ya Wanahisa:-

(a) Mwanahisa hutakiwa kuja na Hati ya Hisa pamoja na kitambulisho chake kinachotambulika (mf; kadi ya Mpiga kura, hati ya kusafiria, Leseni ya Udereva au kitambulisho cha Taifa)

(b) Mwanahisa mwenye udhuru hutakiwa kujaza fomu ya Uwakilishi (Proxy). Fomu hupatikana katika tovuti ya kampuni: www.precisionairtz.com, (Baada ya kufungua tovuti hii nenda katika sehemu ya "*About us*" katika Menu, bonyeza "*investor Relations*". Fomu za uwakilishi zilizojazwa na Mwanahisa zinatakiwa kurejeshwa katika Ofisi za Precision Air Siku Saba (7) kabla ya Mkutano.

(c) Mwanahisa anayehudhuria Mkutano Mkuu hutakiwa kujigharamia mwenyewe.

**13. Mwanahisa: Sijawahi kupata cheti changu cha Mwanahisa, naweza kukipataje?**

**Kampuni**: Hisa za Kampuni yetu zilinunuliwa na Wanahisa kupitia benki za Stanbic na CRDB. Baada ya Wanahisa kununua hisa zao, Vyeti vya Wanahisa (*Share Certificate/ Depository Receipts*) vilitumwa katika benki hizo na kila benki ilituma vyeti hivyo katika Matawi yake mbalimbali nchini (kuzingatia tawi ambalo Mwanahisa alinunulia hisa zake)

Utaratibu wa awali ulikuwa kwamba, Mwanahisa alitakiwa kufika katika tawi la Benki alilonunulia hisa zake akiwa na risiti yake ya malipo na benki ilimpatia cheti chake. Utaratibu huu bado unaendelea kwa Wanahisa walionunua hisa zao kupitia Benki ya CRDB.

Kwa wale Wanahisa walionunua hisa zao kupitia Benki ya Stanbic ambao hawakuchukua vyeti vyao katika matawi ya Benki ya Stanbic waliponunulia hisa zao, utaratibu wao wa kuchukua vyeti vyao ulibadilika baada ya Benki ya Stanbic kurejesha vyeti vyote Precision Air ambavyo vilikuwa havijachukuliwa na Wanahisa ili Precision Air iweze kusimamia ugawaji huo. Kwa hiyo:-

(a) **Kwa Wanahisa walionunua hisa zao za Precision kupitia benki ya Stanbic** ambao hawakufanikiwa kuchukua vyeti vyao pindi vilipokuwa vikitolewa na Benki ya Stanbic kupitia matawi yake, Wanahisa hao wanatakiwa kufuatilia vyeti hivyo katika ofisi zetu za Precision Air. Tuma taarifa zako kamili pamoja na nakala ya risiti ya malipo katika ofisi ya Precision Air iliyo karibu nawe na cheti chako kitatumwa katika ofisi ya hiyo tayari kwa wewe kukichukua au katika sanduku la posta utakalochagua.

(b) **Kwa Wanahisa walionunua hisa zao za Precision Air kupitia Benki ya CRDB** ambao hawakufanikiwa kuchukua vyeti vyao pindi vilipokuwa vikitolewa na Benki ya Crdb kupitia matawi yake, vyeti hivyo vinapatikana katika tawi la CRDB ambalo Mwanahisa alinunulia hisa zake, hivyo Mwanahisa anapaswa kufuatilia Cheti chake huko na kukichukua.

Benki ya Crdb ilipendekeza kutumia utaratibu huo ulioelezwa (wa kusambaza vyeti katika tawi ambalo Mwanahisa alinunulia hisa zake) ili kurahisisha uchukuaji wa vyeti kwa Wanahisa wakiamini kuwa kwa asilimia kubwa makazi ya Mwanahisa husika yalikuwa karibu na tawi la Benki alionunulia hisa zake, hivyo ingesaidia zoezi la kugawa vyeti.

**ANGALIZO**: Wanahisa wanaofuatilia vyeti vyao katika matawi ya benki za Crdb waliponunulia hisa zao hupaswa kwenda na risiti za malipo na kuulizia kuhusu vyeti vya Precision Air na sio ununuaji wa hisa za Precision Air (ambao uliishafungwa).

14. **Mwanahisa**: **Nilipata cheti changu cha Mwanahisa, ila kilipotea/ kiliungua/ kiliibiwa, utaratibu ukoje wa kupata kingine?**

**Kampuni:** Iwapo Cheti cha Mwanahisa kiliibiwa au kupotea, Mwanahisa anatakiwa kuripoti tukio husika katika kituo cha polisi na kupewa “Loss Report” ambayo atatakiwa kuiwasilisha katika Ofisi za Soko la Hisa la Dar es Salaam kwa utaratibu zaidi.

15. **Mwanahisa: Baada ya kununua hisa, nimebadilisha taarifa zangu za msingi (Namba ya akaunti, namba ya simu, sanduku la posta), utaratibu ukoje wa kutoa taarifa mpya (Ku- update)?**

    **Kampuni:** Mwanahisa anapobadilisha taarifa zake za msingi anatakiwa kuijulisha Soko la Hisa la Dar es Salaam ambalo litarekebisha taarifa zake (*update latest information*) katika mfumo wao wa kutunza kumbukumbu (*Database- Central Depository System*) na kutuma taarifa hizi kwenye Kampuni yetu.

    Mwanahisa anayehitaji kubadilisha taarifa zake zozote anatakiwa kutembelea ofisi za soko la hisa la Dar es Salaam au mawakala wake ambapo atapewa fomu maalum ya kujaza taarifa zake za zamani na mpya.

16. **Mwanahisa: Je naweza kulipwa fidia iwapo kampuni yangu inapata hasara mfululizo?**

    **Kampuni:** Hapana, Mwanahisa hawezi kulipwa fidia iwapo kampuni inapata hasara mfululizo. Mwanahisa anayo haki ya kujiondoa katika umiliki wa hisa zake kwa kuuza au kuhamisha hisa zake kwa mtu mwingine kwa kufuata sheria na taratibu za nchi. Pia Mwanahisa anaweza kuvumilia na kusubiri kampuni ikipata faida atapewa gawio lake.

    **ANGALIZO:** Kampuni yetu ni kampuni inayosimamiwa na Mamlaka mbalimbali katika utendaji kazi wake na mahusiano yake na Wanahisa wake. Mamlaka hizi ni kama vile; Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (*Capital Markets and Securities Authority*), Soko la Hisa la Dar es Salaam (*Dar es Salaam Stock Exchange*) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority).

    Mamlaka hizi pamoja na wakaguzi wa nje wa mahesabu ya kampuni hupitia mahesabu yetu na kujiridhisha kuwa hayana udanganyifu wa aina yoyote na kuwa zimefuata utaratibu unaotakiwa kisheria. Hivyo, kupata hasara kwa kampuni ni suala halisi na haliandaliwi au kupangwa na kampuni kwa minajili ya kuwadhulumu Wanahisa wake. Kampuni yetu inajitahidi kwa kila namna kuhakikisha kuwa inatekeleza mipango yake ili iweze kupata faida na hatimaye wanahisa waweze kuvuna kitu katika uwekezaji wao.

17. **Mwanahisa: Je kampuni yangu yaweza kugharamia usafiri, chakula na malazi kwa wanahisa wake wanaohudhuria mkutano wa mwaka wa wanahisa?**
    **Kampuni**: Mwanahisa anayehudhuria Mkutano Mkuu wa Wanahisa anatakiwa kujigharamia mwenyewe usafiri, malazi na chakula. Kampuni haiwezwi kamwe kugharamia mambo haya kwa Mwanahisa anayehudhuria Mkutano Mkuu wa Wanahisa.

**Precision Air Services, Plc**